**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kuanza kuwasilisha Hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenye wingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kutekeleza majukumu yetu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutujaalia amani, upendo, busara na hekima, pamoja na kutuzidishia neema zake zote ambazo ni muhimu katika maisha yetu ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika Mkutano huu wa Kumi na Mbili wa Baraza hili tukufu katika kuuchangia na kuuboresha Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu akuzidishie hekima na busara katika kutekeleza majukumu yako ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, pongezi za dhati kabisa ziende kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Dkt. Mwinyi Talib Haji pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar pamoja na watendaji wa Taasisi mbali mbali za Serikali kwa ushirikiano wao mkubwa wakati Kamati ilipokuwa ikijadili Mswada huu muhimu

kwa ajili ya kuondoa changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sheria husika.

**Mheshimiwa Spika**, pia, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa waliyotoa kwangu na juhudi zao wakati wa kuujadili kwa kina Mswada huu wenye sehemu Kumi na Sita ambazo zimebeba maudhui mbali mbali kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kwa ruhusa yako niwatambulishe Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Maryam Thani Juma | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| *8.* | Mhe. Panya Ali Abdalla | Mjumbe |
| *9.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *10.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *11.* | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| *12.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani wa Lugha za Alama |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inaunga mkono kuwa katika utekelezaji wa sheria, zipo baadhi ya sheria zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili kuondokana na changamoto zinazoipata Serikali katika maeneo mbalimbali ya kiuendeshaji na kiutawala. Hivyo, Serikali kuamua kuwasilisha

mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hizi ni sahihi kwa lengo la kuondosha ugumu uliopo katika utekelezaji wa sheria hizo ambazo zimekuwa kikwazo katika kufikia malengo yake.

**Mheshimiwa Spika,** sina budi kueleza kuwa, hotuba hii itaeleza kwa ufupi baadhi ya maoni ya marekebisho tuliyoyapata ndani ya Mswada huu uliokusanya Sheria Kumi na Sita (16) katika sekta tofauti, ambapo vifungu vingi ndani yake vinafanyiwa marekebisho ili kuweka ubora katika sheria mama baada ya Serikali kuona ipo haja ya kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika *sehemu ya Pili* ya Mswada huu ambayo inahusu marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009 inakusudia kufanya marekebisho katika kifungu cha 2 na 10C kwa lengo la kuimarisha mfumo wa udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi ili kuendana na viwango vya kimataifa. Kamati imeridhika na marekenbisho haya na vile vile, kuitaka Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuzidisha kasi ya kupambana dhidi ya vitendo vya kihalifu vinavyofanywa katika mitandao kwa lengo la kujipatia kipato kwa watu wasiokuwa na uzalendo kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeshauri kufanyiwa marekebisho  Kifungu cha 4 cha Sehemu hii kwa kuingizwa maneno **"ufadhili wa kigaidi"** kila linapojitokeza katika Sheria Mama ambayo imefanyiwa marekebisho katika sehemu ya tafsiri kwa kufuta neno **"ufadhili wa ugaidi"** na kuwekwa badala yake **"ufadhili wa kigaidi"** ili kuleta uwelewa mzuri kwa watumiaji wa Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwenye *sehemu ya Tatu ya Mswada huu ambayo* inahusu marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, Nam. 3 ya  2015. Kwa kuwa Serikali imeamua Sheria hii kufanyiwa marekebisho kwa madhumuni  ya kuweka mfumo mzuri wa kisheria ndani ya sheria juu ya masuala yanayohusiana na baioteknolojia na biashara ya kaboni, basi ni vyema kuhakikisha tumeimarisha mifumo

ya uchunguzi na kuwajengea uwezo wataalamu wetu ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia ulimwenguni kutokana na nchi nyingi sasa kuruhusu matumizi ya vinasaba katika uimarishaji wa mifumo ya chakula na mbolea kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Serikali pia, izidishe nguvu katika kulinda na kuyatunza mazingira ya bahari kupitia meli za mafuta na uvuvi ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikiathiri mazingira ya bahari yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hayo Kamati pia imeshauri kufanya marekebisho madogo katika kifungu cha 30 inayoelezea marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar kwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

a) *Sehemu ya Tano na Kifungu cha 45 cha Sheria Mama vinafutwa.*

b) *Kuzipa nambari mpya Sehemu ya Sita kuwa ya sehemu ya Tano na kifungu cha 46 kuwa cha 45 kwa mpangilio wake.*

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia Marekebisho ya Sheria ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, Nam. 4 ya 2010 ambayo imekwenda kurekebisha Vifungu vya 4 na 6 vitavyopelekea kuondoka kwa vyanzo vya mapato vya Baraza la Mji. Kamati yetu inaunga mkono wazo la Serikali la kuondoa baadhi ya shughuli za Manispaa Mjini na kuhamishia Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe. Hata hivyo, tunaishauri Serikali kuhakikisha inafanya juhudi za kutosha kuwapatia ruzuku Manispaa hiyo ili iweze kutekeleza mipango yake ya kimaendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho ya *Sehemu ya Kumi na Mbili inayohusiana na* Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Nam. 2 ya 2005. Sehemu hii inarekebisha kifungu cha 29 kwa kukifuta na kukiandika upya kifungu kidogo cha (4) (b) kwa mudhumuni ya kuongeza masharti ya mwanachama ya kutolipwa fao la upotevu wa ajira mwanachama ambaye ameacha kazi kwa hiari au ameachishwa kazi kwa kutenda kosa la rushwa, ubadhirifu, wizi au kosa la kinidhamu.

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ambayo imekuwa ikifanyiwa marekebisho mara kwa mara kwa lengo la kuifanya iwe bora na yenye kuondoa changamoto kwa watumishi wa umma. Hivyo, ni imani ya Kamati yangu kwamba sasa umefika wakati kwa watumishi wetu kunufaika zaidi kupitia mfuko huu baada ya kuwekwa fursa nyingi ambazo zinamjali mwananchama katika mazingira tofauti.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kumi na Tano (15) ya marekebisho yanayohusiana na Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011 katika kuwajali na kuwawezesha watumishi hao kuwa na uwezo unaoenda sambamba na mabadiliko ya kila siku, Kamati inaridhia kwa madhumuni ya kuweka utaratibu maalumu wa uhamisho wa watumishi wa umma kwenda nje ya utumishi wa umma wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, Kamati inashauri wakuu wa Taasisi za Umma wasiwe kikwazo wakati watumishi wanapohitaji kutumia fursa hii kwani lengo la Serikali katika marekebisho haya si kuwakomoa watumishi wake katika utendaji bali kuweka uhuru wa watumishi katika utendaji kwa kuwa ni haki yao ya msingi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwashauri wajumbe wa Baraza lako Tukufu wakubaliane na maoni ya Kamati yetu katika Mswada huu kwani Kamati imepata wasaa wa kutosha wa kujadili na kupitia vifungu vya mswada huu kwa msaada wa wataalamu wetu wa Baraza kwa lengo la kuiwezesha Serikali kuzifanyia marekebisho Sheria hizi ili ziwe nyenzo muhimu katika kufanikisha majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, Kamati yetu inawaomba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu waujadili na kuuchangia ipasavyo Mswada huu na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itaziwezesha Taasisi hizi kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika, Naomba Kuwasilisha**.

Ahsante,

……………………………

(*Mhe. Machano Othman Said*)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**